

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA SITA**

**07 JUNI, 2018**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA– TAREHE 07 JUNI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**390. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE  
(MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wakati wa kampeni aliwaahidi Wananchi wa Itigi katika Jimbo la Manyoni Magharibi kusaidia kupunguza gharama kubwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mtakatifu Gaspar, pia kulipa Mishahara yote ya Watumishi, mgao wa dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD), vifaa tiba na kuongeza Madaktari Bingwa:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo;
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kwa sasa ni bora kujenga Hospitali ya Serikali katika Halmashauri mpya ya Itigi.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**391. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, Serikali inajua tatizo la ukosefu wa maji Kilolo linasababishwa na nini na nini suluhisho lake.

**392. MHESHIMIWA SONIA JUMAA MAGOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Tatizo la maji limekuwa sugu sana Wilayani Handeni:-

Je, Serikali imefikia wapi katika kutatua tatizo hili la kunusuru maisha ya Wananchi.

**393. MHESHIMIWA ZAINAB MUSSA BAKAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Maji ni muhimu katika maisha ya mwanadamu na bila maji safi na salama afya za Wananchi zinaweza kuwa hatarini:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Vijiji ambavyo havina vyanzo vya maji hasa ikizingatiwa kuwa bila ya maji safi na salama ni kuhatarisha afya na maisha ya Wananchi hao.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**394. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Gereza la Kilimo la Mng'aro ni miongoni mwa Magereza Kongwe hapa nchini lakini Gereza hili limekuwa na miundombinu chakavu kutokana na umri wake:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kulifanyia ukarabati mkubwa Gereza hili pamoja na kuongeza uwezo wa kuchukua wafungwa wengi zaidi.

**395. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON  
GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Moja ya jukumu la Serikali ni kuhudumia wafungwa kwa maana ya kuwapatia huduma za msingi kama vile chakula, mavazi na matibabu:-

Je, Serikali inafanya nini ili kuhakikisha huduma hizo za msingi katika Gereza la Kasulu zinapatikana kwani wana hali mbaya sana hasa kimavazi.

**DODOMA  
07 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**